**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 03 Oktoba, 2023**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2020/2021.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya mwaka 2020/2021.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

90. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Kwa kiasi kikubwa Serikali inategemea mifumo mbali mbali, ikiwemo ya manunuzi na ukusanyaji wa mapato, katika kuboresha ufanisi na utendaji kazi za kila siku za Serikali. Hata hivyo, kumekuwa na manung’uniko na wasiwasi juu ya utayari wa Serikali katika dhana mzima ya Serikali Mtandao.

(a) Je, Serikali imejiridhisha vipi kuhusu umakini na ufanisi wa mifumo hiyo.

(b) Je, usalama wa kila siku uko vipi na utumiaji wa mifumo hiyo kwa wale wanaopitishia malipo na taarifa muhimu katika mifumo hiyo.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

67. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa za kutunga sheria mbali mbali zinazohusiana na Mabaraza ya Miji na Halmashauri mbali mbali nchini, lakini utekelezaji wa sheria hizo haufanani na malengo yaliyokusudiwa, hali inayosababishwa na utekelezaji wa sheria zinazosimamiwa na Wizara yako mara nyingi huonekana kama zinadhoofisha sheria za Mabaraza ya Miji na Halmashauri zilizo chini yake.

Je, ni lini Serikali italitatua jambo hili na kuleta usawa wa sheria za Wizarani na zile za Mabaraza ya Miji na Halmashauri zilizo chini yake.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

105. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Tunaipongeza Serikali katika kusaidia kupatikana ajira kwa wananchi wake. Kwa kuwa kwa mwaka 2022 jumla ya ajira zilizopatikana zilikuwa 68,632 kutoka sekta mbali mbali, ambapo ajira za Serikali pekee zilikuwa 37,189. Na kwa kuwa kati ya ajira hizo za Serikali, ajira zilizopatikana kwa wanaume zilikuwa 15,541 na wanawake ni 21,648. Na kwa kuwa kwa upande wa Mashirika ya Serikali zilikuwa 6,887, ambapo kwa upande wa wanaume zilikuwa 4,522 na wanawake ni 2,365.

(a) Je, ni ajira ngapi za Serikali na watu binafsi zimepatikana tokea mwaka wa 2020 hadi 2023.

(b) Je, ni mgawanyiko upi wa ajira kwa kila Wizara na ajira ngapi zimepatikana kati ya hizo.

(c) Je, ni ajira ngapi za Sekta Binafsi zilizopatikana kwa mwaka 2022.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

108. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mapungufu katika udhibiti wa mifumo ya ndani ni hoja inayojitokeza mara kwa mara katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa taasisi nyingi za Serikali.

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuondoa hoja hii.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

101. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habaril, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, inastahili pongezi kwa kazi nzuri ya kuimarisha miundombinu ya michezo hasa katika ujenzi wa viwanja vipya na ukarabati wa viwanja vikongwe vya Amani na Gombani.

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuvikarabati viwanja vya Mao tse tung ili viwe katika hali bora zaidi ya ilivyo hivi sasa.

(b) Je, mpango huo unategemewa kuanza lini.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

114. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ibara ya 182 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaielekeza Serikali kukamilisha madarasa ya skuli yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Je, lini banda la vyumba vinne vya madarasa ya skuli ya msingi Wawi litakamilishwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

112. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni Serikali ilianza kufanya tathmini ya fidia kwa wananchi watakaoingia kwenye eneo litakalohusika na utanuzi wa uwanja wa ndege Pemba.

(a) Je, tathmini hiyo imekamilika.

(b) Ni kiasi gani kitatumiwa kulipa fidia kwa wananchi hao.

116. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Je, ni lini ahadi ya kuweka taa za barabarani katika eneo la Machomane Pemba itatimizwa.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2020/2021.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya mwaka 2020/2021.

**Zanzibar,**
**03 Oktoba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**